

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma Kuongeza Ufanisi

UTANGULIZI

Katika Mwaka wa fedha 2014/15 Serikali imeandaa Mwongozo wa Usimamizi na Utayarishaji wa Miradi ya Uwekezaji katika sekta ya Umma (Public Investment Management Operational Manual) kwa lengo la kuimarisha utendaji, uwajibikaji na kuleta ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma zinazoelekezwa katika miradi ya maendeleo. Shabaha kuu ya mwongozo huu ni kutoa maelekezo ya mchakato na hatua zinazohitajika kufuatwa katika kutayarisha na kutekeleza miradi yote inayotumia fedha za umma au kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mwongozo unazielekeza Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa jinsi ya kufanya uchambuzi unaozingatia vigezo vya kiuchumi na kifedha na kufafanua mbinu, hatua, taratibu, na kuweka viwango vinavyohitajika katika kuandaa na kuwekeza miradi.

Maelekezo ya mwongozo huu yanafafanua vigezo muhimu vya uchambuzi wa kiuchumi na kifedha ili kufikia uamuzi wa miradi ipi ina manufaa na inaweza kupata mikopo katika soko la mitaji la ndani au la kimataifa.

Hivyo, vigezo kama mzunguko wa mradi (project cycle) ikiwa ni pamoja na andiko la awali (concept note), mchanganuo wa faida na hasara (cost-benefit analysis) vigezo vya kuchanganua mradi kama vile uwezo wa uzalishaji (internal rate of return) na thamani halisi ya uwekezaji (Net Present Value), na vinginevyo vimeainishwa vizuri katika Muongozo.

Katika hili utaalumu unahitajika wa uchambuzi wa mizania ya gharama na faida za miradi inayopendekezwa kwa kutumia vigezo vya kifedha au kiuchumi. Mfano riba, mabadiliko ya bei za soko, maoteo ya mtiririko wa gharama mbalimbali, faida au athari za miradi za kiuchumi, kijamii au kimazingira

Kwa sasa miradi yote itakayohitaji fedha za Serikali katika Bajeti italazimu kufuata utaratibu uliobainishwa katika mwongozo huu ili kuweza kuimarisha ufanisi na kupata thamani ya fedha. Hivyo, Mwongozo ni chombo muhimu katika michakato mbalimbali ya kupanga bajeti kama vile Mwongozo wa Mpango na Bajeti (unaotolewa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango kila mwaka), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka Mmoja (unaotolewa na Tume ya Mipango), na kadhalika.

Wahusika Wakuu wa Mwongozo

Walengwa wakuu wa mwongozo huu ni wataalam wote walio chini ya idara za Sera na Mipango na zile za uwekezaji katika mashirika na taasisi mbalimbali za umma. Aidha, viongozi (katika ngazi zote) ambao ni watoa maamuzi hawana budi kuelewa Mwongozo huu ili kutoa maamuzi sahihi.

Watumiaji wengine muhimu wa Mwongozo huu ni pamoja na wawekezaji kati ya sekta ya umma na binafsi, wabunge, washirika wa maendeleo, wachambuzi wa fedha na uchumi, asasi za kiraia na umma kwa ujumla.

Mpangilio wa Kitabu cha Mwongozo

Kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji katika Sekta ya Umma kimegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya awali na mtiririko wa kuandaa mwongozo huo (Background information and flow of PIM management), sehemu ya pili inaeleza kuhusu utambuzi wa miradi na mipango yake (Project identification and Planning), sehemu ya tatu inaeleza juu ya ufadhili wa miradi na usimamizi (Financing and management), sehemu ya nne inaelezea kuhusu ufuatiliaji na tathimini ya miradi na sehemu ya tano inaelezea kuhusu kanzi-data ya miradi na mfumo wa kutoa taarifa (Database and reporting format).

Kujenga Uwezo na Mfumo wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Miradi ya Uwekezaji wa Umma

Mwongozo huu pia unategemewa kuwa mwanzo wa kujenga uwezo katika usimamizi wa uwekezaji wa umma. Hivyo basi utakuwa ni msingi wa kuwaimarisha maafisa wa serikali kinyenzo katika kuchambua, kuchagua, kuwasilisha miradi ya uwekezaji kiuchumi na kifedha, pia kijamii kwa kukidhi taratibu na sheria zinazoendesha uwekezaji katika sekta ya umma.

Katika kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo huu na kujenga uwezo wa kutosha, Serikali imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa walengwa wakuu katika ngazi za mafunzo ya muda mfupi, muda wa kati na mrefu ili kuongeza utaalum na kuwekeza miradi michache kwa mwaka wa bajeti lakini kwa ufanisi zaidi.

Mwongozo pia unatoa taratibu kwa miradi ambayo haitapata fedha kwa mwaka husika itawekwa katika kanzi-data (Database) ambayo itaanzishwa chini ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa ajili ya kufikia malengo ya utekelezaji wa usimamizi wa uwekezaji katika sekta ya umma.

Kukamilika kwa *database* kunaweza pia kupunguza miradi na ahadi nyingi ambazo wananchi wanapata kupitia viongozi katika kampeni mbalimbali na badala yake ahadi hizo zitatokana na *Database* ambayo inaonyesha miradi gani ya umma, itaanza lini, na kumalizika lini na ina fedha kiasi gani. Hivyo, zoezi hili litasaidia pia wanasiasa katika shughuli zao za kila siku kwa kufuata Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na mipango mbalimbali ya kitaifa.

Muda wa Utekelezaji

Mwongozo unatarajiwa kutolewa kwa ajili ya matumizi na utekelezaji wake kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2014/15.

Imetolewa na

Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango